**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO**

**SIMU:**
Mkuu wa Shule:
0768078372/0675572663
Makamu Mkuu wa Shule:
0752564226/0698853031.

SHULE YA SEKONDARI KAKONKO BOYS
S.L.P 03,
**KAKONKO,**

TAREHE …………………………….

MZAZI/MLEZI WA ………………………………………….....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KAKONKO BOYS, WILAYA YA KAKONKO MKOA WA KIGOMA ……………….**

## 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano mwaka …………… katika Shule ya Sekondari Kakonko boys tahasusi ya (HGK, HGL). Shule hii ni shule ya bweni na ipo katika kijiji cha Kasanda, Wilaya ya Kakonko, katika Mkoa wa Kigoma, na ipo umbali wa kilometa 5 kutoka kwenye kitovu cha Kijiji cha Kasanda. Usafiri wa bodaboda kutokea kituo cha mabasi cha Kasanda ni shilingi 5000/=. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 06/07/2026, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 06/07/2026.

## 2.0. MAVAZI

### 2.1. SARE ZA SHULE

i. Suruali mbili za bluu nyeusi (dark blue) za darasani zenye mifuko mitatu na tai ndefu ya rangi hiyo ya dark-blue. Na suruali zote lazima ziwe na marinda, tanapu ya chini na ziwe na upana wa chini inch 17. (**SURUALI ZA MODEL HAZIRUHUSIWI**). (suruali hizo zitapatikana shuleni kwa bei nafuu)

ii. Nguo za kushindia(shamba dress) ni suruali mbili za rangi ya ugoro zenye mifuko mitatu. Na suruali zote lazima ziwe na marinda, tanapu ya chini na ziwe na upana wa chini inch 17. (**SURUALI ZA MODEL HAZIRUHUSIWI).** (suruali hizo zinapatikana shuleni kwa bei nafuu)

iii. Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu zisizo na mapambo yoyote wala zisibane zenye vifungo vya kawaida.

iv. Soksi nyeusi jozi mbili.

v. T-shirt za shule mbili za rangi ya kijani nyeusi (dark green) zenye kola nyeusi na Nembo ya shule zitapatikana shuleni kwa bei nafuu.

vi. Sweta rangi ya bluu nyeusi (dark blue) itapatikana shuleni kwa bei nafuu.

vii. Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu, vyenye Kamba, na visigino vifupi. (Bajaji na yeboyebo haziruhusiwi kabisa).

viii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali ix. Kanda mbili kwa ajili ya kuogea na viatu vya wazi kwa ajili ya kuvaa baada ya mda wa masomo x. Vesti mbili nyeupe.

xi. Full tracksuit kwa mwanafunzi rangi ya bluu yenye mchirizi mweupe. (Ataripoti akiwa amevaa)

N: B Nguo nyingine zozote mbali na sare za shule zilizotajwa hapo juu **HAZIRUHUSIWI.**

**2.1 SARE ZA MICHEZO**.

i. Raba nyeusi moja ya michezo kwa wanafunzi wote,

ii. Kaptula na T-shirt rangi bluu nyeusi (dark blue) jozi mbili,

**3.0 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAYO SHULENI-**

**3.1. VIFAA VYA MASOMO.**

i. Daftari 10 (counter books quire 4)

ii. Rim 2 A4 “double A”.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika aliyochaguliwa mwanafunzi. **(*Tunashauri anunue Vitabu vilivyopo chini ya (TIE)***

**3.2. VIFAA VYA USAFI.**

Aje na mfagio (hard broom, floor squeezer), Ndoo mbili za lita kumi, Fyekeo, Jembe na Reki.

### 3.3 MALAZI

i. Mwanafunzi aje na Mashuka mawili ya rangi ya bluu bahari, Aje na chandarua rangi ya bluu bahari, Blanketi nzito, Sanduku la chuma la kutunzia vitu vyake( trunker).
ii. Godoro linapatikana shuleni kwa bei nafuu kwa kukodi kwa mwaka hivyo mwanafunzi asije na godoro.

### 3.4 MAHITAJI MENGINE

i. Kila mwanafunzi aje na vyombo vya chakula yaani sahani moja, bakuli moja, kikombe na kijiko kimoja.
ii. Kutokana na hali ya udongo wa shuleni mwanafunzi anatakiwa kuja na mabuti ya mvua (gumboots).

**NB; Mwanafunzi aje na bima ya afya ili imsaidie katika gharama za matibabu kwa kipindi awapo shuleni.**

## 4.0 MICHANGO MBALIMBALI

| No. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji | 65000 |
| 2 | Tahadhari | 5000 |
| 3 | Nembo | 5000 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5000 |
| | Jumla | 80000 |

Michango hiyo ilipwe kwenye akaunti **No: 0150000UE5S00, CRDB** jina la akaunti **KAKONKO BOYS SECONDARY SCHOOL** aje na risiti ya malipo ya benki afikapo shule.

## 5.0. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

### 5.1. MAMBO YA KUZINGATIA SHULENI

i. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa ni muhimu.
ii. Kuwahi katika kila shughuli ya shule atakayopangiwa.
iii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo shule hii Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
iv. Kuvaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni na nje ya shule na anapokuwa kwenye shughuli za kitaaluma.
v. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote, Sare za shule huvaliwa wakati wote ukiwa shuleni, wakati wa kwenda nyumbani, na wakati wa kurudi shuleni.
vi. Lugha ya mawasiliano awapo shuleni kwa muda wote ni kiingereza.

vii. Mwanafunzi awe na bidii ya kujielimisha na kufanya mazoezi na majaribio yote darasani na mitihani yote ikiwemo ya nje.
viii. Kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu wastani wa alama 70%.
ix. Kila mwanafunzi atawajibika kulinda na kutunza mali ya shule na yake binafsi.
x. Kwa Mwanafunzi atakaye haribu mali ya shule kwa Maksudi, atapaswa kulipa mara moja baada ya kuthibitika.

xi. Kila mwanafunzi analazimika kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika maongezi na walezi wake pasipo kutumia lugha chafu.
xii. Kutokuwa na chakula cha aina yoyote bwenini.

**5.2. MAKOSA YA KUWEZA KUKUFUKUZISHA SHULE**

i. Wizi.
ii. Kugoma na kuhamasisha mgomo. iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, au mtu yeyote yule. iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
v. Ulevi au unywaji wa pombe, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji wa sigara.
vi. Uasherati, uhusiano wa kimapenzi jinsia moja, kuoa .
vii. Kushiriki, matendo ya uharifu,siasa na matendo yoyote yanayo vunja sheria za nchi. viii. Kutembelea majumba ya starehe (Baa, Kumbi za muziki) na nyumba za kulala wageni (Guest House). ix. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu za mkononi, Laini au kukutwa na chaja ya simu katika mazingira ya shule.
x. Kunyoa mitindo (panki, kiduku, kipara) na kufuga ndevu.
xi. Kudharau bendera ya Taifa.
xii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu, na Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**6.0 VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu; na
v. Kivuli cha matokeo ya kidato cha IV (result slip) na Cheti cha kuzaliwa.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA.

**MOTO: BE HAPPY, BE ENERGETIC, BE YOU, THINK SCHOOL.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KAKONKO BOYS.**

**ROGERS MUTALEMWA KILLO.**

**MKUU WA SHULE.**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI.**

1. Jina la mwanafunzi…………………………………………………………..

2. Jina la baba …………………………………………………………………..

3. Jina la mama………………………………………………………

4. Jina kamili la mlezi ……………………………………………………….

5. Anuani ya mzazi/mlezi…………………………………………………..

6. Uhusiano wa mlezi………………………………………………………..

7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) 8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni……………………………………………………….……………

9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni.......................................................

10. Kama ni mfanya kazi, kazi yake ni………………………………………………

11. Afya ya mwanafunzi, Kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum. Tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
… ………………………………………………………………………………..

12. Madhehebu ya dini ………………………………………………………………..

13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi.

i. …………………………………………………………………………

ii. …………………………………………………………………………

iii. …………………………………………………………………………

iv. ……………………………………………………………………………

**KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.**

Jina la mwanafunzi………………………………………………………………………………

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………………………….

Anuani ya mzazi/mlezi ………………………………………………………………..

Uhusiano …………………………………(mjomba, shangazi, kaka, dada).

Mimi ………......................................................................nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanfunzi wa Tanzania naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo ninaahidi kuwa nitajibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni,nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi. Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na ninaahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria. Nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………………

Tarehe………………………………..........................

Mimi …………………………………………………………mzazi/mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………………… ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlezi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.

Sahihi ya mzazi/mlezi……………

Tarehe……………………………

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

Students name…………………………………………………………………………………

Age …………………………………………..

Stool test………………………………………………………………………………

Blood group……………………………………………………………………………

Urine analysis…………………………………………………………..

Sphills test ………………………………………………………..

Chest test………………………………………………………………………………

Speech………………………………………………

Eye test ………………………………………………..

Abdomen………………………………………………

Additional information and physical defect or impairment to pursue further education.

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………
… ……………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

Signed …………………………………………………

Designation ……………………………………………….

Official stamp

Date…………………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA TAMISEMI.**

**SHULE YA SEKONDARI KAKONKO.**

**AHADI YA MZAZI:**

Mimi…………………………………………………………………..……………………. (Jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi wa …………………………..………………………… kidato cha…………………………

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema.Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii.Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia mwanangu malezi na elimu bora kwa manufaa ya Taifa la Tanzania.Na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapo takiwa kufanya hivyo.Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria,kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

Saini ya mzazi/mlezi ………………………

Anuani kamili…………………………

Simu………………………

Tarehe……………………